**NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU**

**1 JULAI 2013**

Kwa Washiriki wa Mikutano 114 ya Vijana inayokuja duniani kote
Marafiki Wapendwa sana,

Wakati Mtukufu Bab, akiwa na umri wa miaka ishirini na tano tu, alipoinuka ili kuwasilisha ulimwenguni ujumbe Wake wa ubadilishaji kabisa, wengi miongoni mwa wale ambao walikubali na kusambaza mafundisho Yake walikuwa ni vijana, wengine hata wadogo kuliko Bab Mwenyewe. Ushujaa wao, umepata maisha ya milele kwenye mwangaza mkali sana katika "Waleta Mapambazuko" na utaangaza kumbukumbu za kihistoria kwa karne nyingi zijazo. Hivyo ulianza mtindo ambao kwao kila rika la vijana, wakipata kutiwa moyo kutoka kwenye msukumo uleule wa kiroho ili kuutengeneza upya ulimwengu, walitwaa fursa kuchangia kwenye hatua mpya katika mchakato unaokunjuka ambao utabadilisha maisha ya walimwengu. Ni mtindo ambao haukuruhusu pingamizi lolote, tokea wakati wa Bab hadi wakati huu wa sasa.

Bidii katika maisha yao yote na kujitoa muhanga kwa ndugu zenu wa kiroho waliotangulia kumefanya mengi kustawisha Imani katika nchi mbalimbali na kuharakisha kutokea kwa jumuiya ya kiulimwengu yenye azma. Ingawa kazi ambayo iko mbele yenu sio sawa kama yao, wajibu ambao mnakabidhiwa, umuhimu wake haujapungua. Baada ya miongo mingi, kazi inayokumbatia dunia ya jumuiya hii iliyoenea sana, ya kupata ufahamu wa kutosha wa Ufunuo wa Baha'u'llah na kufanyia kazi kanuni ilizozihifadhi imeishia katika kuibuka kwa mfumo wenye uwezo kwa ajili ya utendaji, ulioboreshwa kupitia uzoefu. Ninyi mna bahati kuwa na uzoefu wa mbinu zake na mitazamo ambayo sasa imeshamiri vizuri. Kwa kupitia ustahimilivu katika utekelezaji wake, wengi wenu mtakuwa tayari mmejionea wenyewe dalili za nguvu ya ujengaji jamii ya mafundisho ya kiroho. Katika mkutano mnaohudhuria, mnakaribishwa kufikiria mchango ambao unaweza kutolewa na kijana yeyote anayetaka kuitikia mwito wa Baha'u'llah na kusaidia kufungulia nguvu hizo. Ili kuwasaidia, idadi kadhaa ya mada zimechaguliwa kwa ajili yenu kuzichunguza, mkianza kwa kuangalia wakati uliopo wa maisha yenu.

Ulimwenguni kote watakusanyika, katika korija nyingi za mikutano ya vijana wakishirikiana malengo yale yale, makumi ya maelfu ambao wana mengi yanayofanana. Ingawa uhalisia wenu unaundwa na tofauti pana ya kimazingira, hata hivyo hamu ya kuleta mabadiliko endelevu na uwezo wa huduma ya maana, vyote viwili ni tabia bainishi kwenye hatua yenu ya maisha, havina ukomo ama kwa mbari au kwa taifa lolote, wala havitegemei kwenye uwezo wa vitu. Kipindi hiki king'aacho cha ujana mnachoshiriki hupitiwa na wote – lakini ni kifupi, na hutumiwa vibaya na idadi kadhaa ya nguvu za kijamii. Hivyo, ni muhimu kiasi gani kujitahidi ili kuwa miongoni mwa wale ambao, katika maneno ya 'Abdu'l-Baha, "waliochuma tunda la maisha."

Tukiwa na hilo akilini, tuna furaha kwamba wengi kati yenu tayari mnashiriki katika huduma kwa kuendesha shughuli zijengazo jumuiya, na pia kwa uanzishaji, uratibu, au kwa kuongoza juhudi za wengine; katika jitihada zote hizi mnabeba kiwango kiongezekacho cha majukumu kwenye mabega yenu. Sio cha kushangaza, kuwa ni kundi la umri wenu ndilo linalopata uzoefu zaidi katika kuwasaidia vijana chipukizi, na watoto pia, katika maendeleo yao ya kiroho na kimaadili, kukuza ndani yao uwezo wa huduma ya pamoja na urafiki wa kweli. Baada ya yote, kwa kufahamu kuhusu ulimwengu ambao roho hizi changa zitahitaji kupitia, pamoja na hatari ilizonazo na pia fursa zake, ninyi tayari mnathamini umuhimu wa kujiimarisha kiroho na kujitayarisha. Kwa kufahamu, kama mlivyo, kwamba Baha'u'llah alikuja ili kubadilisha vyote maisha ya ndani na hali za nje za wanadamu, ninyi mnasaidia wale wadogo kuliko ninyi kuboresha tabia zao na kujitayarisha ili kuchukua wajibu kwa ajili ya ustawi wa jumuiya zao. Kadiri wanavyoingia ujana, mnawasaidia kukuza uwezo wao wa kujieleza, pamoja na kuwezesha hisia imara ya kimaadili kuanza kuota mizizi ndani mwao. Katika kufanya hivyo, hisia yenu wenyewe ya azma inajiunda vyema zaidi kadiri mnavyosikiliza amri ya Baha'u'llah: "Acha vitendo, sio maneno viwe pambo lenu."

Kufuata njia ya huduma, katika hali yoyote ambayo shughuli zake mtu huchukua, inahitaji imani na uthabiti. Katika muunganiko huu, faida ya kutembea katika njia hiyo kwa kuambatana na wengine ni kubwa sana. Kuambatana kwa upendo, kutiana moyo pande zote mbili, na kuwa tayari kujifunza kwa pamoja ni sifa za kiasili za kikundi chochote cha vijana ambacho kinajitahidi kwa dhati kufikia malengo sawa, na hazina budi kubainisha mahusiano yale ya msingi ambao huunganisha pamoja viungo vya jamii. Kutokana na hili, tunatumaini muungano mliouanzisha kupitia ushirikiano na washiriki wengine wa mkutano utathibitisha kuwa wa kudumu. Naam, muda mrefu hata baada ya kufungwa kwa mikusanyiko hii, huwenda vifundo hivi vya kirafiki na mwito wa pamoja vitawaasaidia kusimama imara.

Uwezekano uliowasilishwa kwa utendaji wa pamoja huonekana wazi hasa katika kazi ya ujenzi wa jumuiya, mchakato ambao unapata mwendokasi katika klasta nyingi na katika ujirani na vijiji ulimwenguni kote ambazo zimekuwa vituo vya shughuli za nguvu. Vijana mara nyingi huwa mstari wa mbele kwa kazi kwenye mielekeo hii – sio vijana wa Ki-Baha'i pekee, lakini pia wale wenye mawazo yanayofanana nao ambao wanaweza kuona athari chanya za yale ambayo Wa-Baha'i wameyaanzisha na kupata maono ya kimsingi ya umoja na mabadiliko ya kiroho. Katika sehemu kama hizo, umuhimu wa kushirikiana Ufunuo wa Baha'u'llah na wale wenye mioyo pokevu na kuchunguza maana za ujumbe Wake kwa ulimwengu wa leo, uhisiwa kwa kina. Wakati sehemu kubwa ya jamii inakaribisha hali ya utepetevu na kutojali au, mbaya zaidi, kuhamasisha tabia ambazo ni za kuwadhuru wao wenyewe na wengine, tabia tofauti za kupendeza zinatolewa na wale ambao wanakuza uwezo wa watu ili kukuza na kuendeleza ustawi wa mfumo wa maisha ya jumuiya utajirishao kiroho.

Hivyo, ingawa wengi wanapendezwa na uwezo na mawazo yenu, umuhimu wa kweli wa jitihada hizi hauko wazi sana kwa ulimwengu kwa ujumla. Hata hivyo, ninyi, mnatambua nafasi yenu katika mchakato mkuu, ubadilishao, ambao muda ukifika, utazaa ustaarabu wa ulimwengu unaoakisi umoja wa binadamu. Mnafahamu vyema kwamba tabia za akili na moyo ambazo mnazilea kwenu wenyewe na kwa wengine zitadumu, zikitoa ushawishi katika maamuzi yenye matokeo ambayo yatahusiana na ndoa, familia, masomo, kazi, hata wapi pa kuishi. Ufahamu wa muktadha huu mpana, husaidia kuvunjavunja kioo cha kujitazamia kinachopotosha ukweli ambacho kwacho majaribu ya kila siku, shida, vipingamizi, na kutoelewana vinaweza kuonekana kama visioshindika. Na katika mapambano ambayo ni ya kawaida katika ukuaji wa kila mtu kiroho, dhamira inayohitajika ili kufanya maendeleo ni rahisi kuitwa wakati nguvu za mtu zimeelekezwa kwenye lengo la juu – itawezekana zaidi wakati mtu anayehusika yuko kwenye jumuiya ambayo ina umoja katika lengo lile.

Mawazo haya yote ni mwanzo wa mazungumzo ya pamoja na yanayoendelea kupanuka ambayo yatazidi kwa kupitia mikutano na hata zaidi ya hapo kwa kadiri mnavyoshirikisha wengine katika mazungumzo ya bidii ambayo huinua moyo na kuamsha akili kwenye uwezekano wa nini kinaweza kuwa. Kuchota kutoka kwenye uzoefu wenu wa pamoja kutatajirisha majadiliano yenu zaidi. Katika muda huu wa heri, mioyo yetu itakuwa pamoja nanyi, na kadiri kila mkutano utakapomalizika, tutakuwa tunaangalia kwa shauku ni nini kitakachofuata. Kwa kila mkusanyiko tutamsihi Mwenyenzi kutoa kwa washiriki wake kiasi cha rehema Yake isiyo na mpaka, tukifahamu, kama mnavyofahamu, kwamba msaada wa mbinguni umeahidiwa kwa wote ambao watainuka kuhudumia binadamu katika kuitikia mwito wa kuamsha wa Baha'u'llah.

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu